# *Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo*

## 1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 AGOSTI, 2026 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 AGOSTI, 2026

### 1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE 11-20 AGOSTI, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilidhohofika. Hali hii ilidumisha mwenendo wa ukandamvua kuwepo kaskazini zaidi, nje ya nchi yetu. Aidha, mifumo ya hali ya hewa iliyopo katika ukanda wa ziwa Victoria pamoja na upepo wa bahari wenye unyevu unyevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki viliimarisha kwa vipindi vichache mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

### 1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 AGOSTI, 2026

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, wakati kwa upande wa ukanda wa pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki vipindi vya mvua vilijitokeza.

## 2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-31 AGOSTI, 2026

### 2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 AGOSTI, 2026

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kudumisha mwenendo wa ukandamvua kuwepo kaskazini zaidi, nje ya nchi yetu. Aidha, mifumo ya hali ya hewa iliyopo katika ukanda wa ziwa Victoria pamoja na upepo wa bahari wenye unyevunuevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani vinatarajiwa kuimarisha kwa vipindi vichache mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727F_03/2026*

**2.2 MWELEKEO WA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-31 AGOSTI, 2026.**

**Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Mvua zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Hali ya ukavu inatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Imetolewa na:

***MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA***

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz